

POLISI WANACHOWEZA KUSEMA?

Polisi wanaweza kutumia maneno kama vile 'yasiyo ya tuhuma za upotevu' au 'zisizo na tuhuma za kifo'. Ishara hizo zinaweza kumaanisha kwamba mtu unayemtafuta emetoweka kutokana na uhalifu. Sababu ya kufanya mtu kukosekana haielezeki mpaka kuwe ushahidi wa kueleza sababu ya kupotea.



VICTORIA POLICE YAKO

- Kama unajua alipo ya mtu ambaye imeripotiwa kuwa ametoweka, au una habari yoyote juu ya kukosekana mtu, piga Crime Stoppers kwa **1800 333 000**.
- Victoria Police hutoa huduma ya bure ya jamii.
- Msaada wa Victoria Police unapatikana masaa 24 kwa siku, siku.
- Polisi katika Victoria huvaa sare ya bluu au nguo za kawaida.
- Wanachama wa umma wanaweza kuhudhuria vituo vya polisi kuripoti matukio au kutafuta ushauri.
- Victoria Police inaweza kutoa wakalimani, pale inapostahili.
- Anwani na namba za simu kwa vituo vya polisi vya mahali vinaweza kupatikana katika www.police.vic.gov.au.



VICTORIA POLICE

www.police.vic.gov.au



VICTORIA POLICE



KUTOA TAARIFA YA MTU ALIYEPOTEA

**KUPATA MSAADA WA POLISI
KAMA MTU UNAYEMJUA
AMEPOTEA.**

Kama una wasiwasi juu ya usalama wa mtu ambaye haonekani, unaweza kutoa ripoti yao kama watu waliopotea kwa polisi wa eneo lako kwa kufanya kile kinachoitwa 'ripoti ya mtu aliyepotea'.

**HAUHITAJI KUSUBIRI MASAA 24 KUWEZA
KUTOA RIPOTI YA MTU ALIYEPOTEA.**

**UNAWEZA KUTOA RIPOTI YA MTU
ALIYEPOTEA HARAKA MARA MOJA.**



JINSI YA KUFANYA RIPOTI YA MTU ALIYEPOTEA

Ili kuripoti mtu kama kapotea, fina katika kituo cha polisi cha karibu.

POLISI WATAKUULIZA MASWALI YANAYOFUATA:

- Mtu aliyepotea anaonekana namna gani?
- Je mtu huyo ana kitu chochote cha tofauti kwa jinsi anavyoonekana?
- Je una picha ya hivi karibuni ya mtu aliyepotea?
- Wapi na lini mtu huyo alionekana au kusikika?
- Je kuna maeneo ambayo mtu aliyekosekana huwa anatembelea mara nyingi?
- Je, mtu huyo ana matatizo yoyote ya matibabu au kuhitaji dawa yoyote?
- Ni majina na namba za kuwasiliana zipi za jamaa na marafiki wanaohusiana na mtu huyo?
- Je mtu aliyepotea anaweza kuzungumza Kiingereza?



INAKUWAJE MTU KUCHUKULIWA KUWA 'AMEPOTEA'?

MTU AMEPOTEA KAMA:

- Wametolewa taarifa polisi na kwamba mahali walipo hapajulikani; na
- kuna woga juu ya usalama au maisha ya mtu huyo.



JE UNAHITAJI MSAADA KATIKA KUFANYA RIPOTI HII?

Pale inapowezekana, unaweza kuomba kuwepo kwa afisa wa jinsia moja na yako mwenyewe wakati wa kufanya ripoti hii.

Polisi watakuuliza wewe jina lako na anwani ili waweze kuendelea kuwasiliana na wewe kuhusu mtu aliyekosekana.

Kama Kiingereza sio lugha yako ya kwanza, polisi wanaweza kutoa wataalamu wa ukalimani wa simu ili kukusaidia na maamuzi ya ripoti hii. Hii ni huduma ya bure. Mkalimani wa simu anaweza pia kukusaidia kuelewa maneno fulani polisi wanayoweza kutumia. onsite (uso kwa uso) Mtaalamu wa ukalimani wa mahali (uso kwa uso) pia anaweza kutolewa kama inatakiwa, hata hivyo, hii ni huduma inayopangwa kabla katika tarehe na wakati mzuri kwa sehemu zote ukijumuisha polisi, mkalimani na mtu kufanya ripoti hii.